# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

Bila kujali hali ya uhamiaji, batu bote mu inchi ya Marekani bako na haki zenye zinalindwa na kuhakikishwa na Katiba. Hii mwongozo imetayarishwa kwa kujulisha batu benye habako banainchi ba Marekani kuhusu haki zao za kisheria mu hali mbalimbali wakati banakutanana na maafisa wa sheria na maafisa wa uhamiaji.

Sheria za majimbo **fulani** zinaweza kutofautiana. Sheria tofauti zinatumika mu **vituo ya ukaguzi** na wakati ya kuingia Marekani kupitia fasi rasmi za kuingilia mu inchi, sawa vile ku mipaka na ku viwanja ya ndege.

**Hii maelezo imetolewa kwa malengo ya elimu na haipashwi kutumiwa ku nafasi ya msaada wa kisheria. Kama weye ao mutu mwenye unajua anahitaji msaada wa kisheria, tafazali wasiliana na mwanasheria.**

## KAMA AFISA WA UTEKELEZAJI WA SHERIA AO AFISA WA UHAMIAJI ANAKUSIMAMISHA UKIWA MU GARI YAKO

### MU HALI ZOTE ZA KUSIMAMISHWA:

- Polisi ao maafisa wa uhamiaji banaweza kukuambiya usimamishe gari, kwa kawaida kwa kukuwakisha matala ao kulilisha sireni ya gari ya polisi. Kama inakufikiya, wakisha matala ya tahazari, punguza mwendo, na usimamishe gari pembeni ya barabara haraka iwezekanavyo. Simamisha gari fasi ya batu bote kwenye kuko mwangaza ya kutosha na usalama.
- Zimisha injini, wakisha matala ya ndani ya gari, fungula dirisha kidogo, na utiye mikono yako ku usukani.
- Dereva na bengine benye bako mu gari bako na haki ya kubakiya kimya. Kama uko musafiri mu gari, unaweza kuuliza kama uko huru kuenda. Afisa akisema ndiyo, enda kwa utulivu.

### KAMA POLISI BANAKUSIMAMISHA:

- Bapolisi bakikuuliza jina yako na leseni ya udereva, unapashwa pana zile habari.
- Ubaulize: "Juu ya nini nimesimamishwa?" Unaweza pia kuuliza: "Je, niko huru kuenda?" Kama jibu ni ndiyo, funga dirisha polepole na uende kwa utulivu.
- Wakati bapolisi banakusimamisha juu ya kosa ya mu barabara, banaweza kukulomba leseni ya udereva, barua ya usajili wa gari, na uthibitisho wa bima. Kama uko na zile barua, unapashwa zionyesha.
- Bapolisi bakikulomba leseni ya udereva, usajili ya gari, na uzibitisho ya bima, unapashwa onyesha zile barua.
- Usijibiye maswali kuhusu mambo ingine, ikiwa amo hali yako ya uhamiaji ao inchi kwenye unatokea. Sema: "Sipendi kujibiya ile maswali."
- Bapolisi, hapana maafisa wa uhamiaji, banaweza kukagua gari kama bako na sababu ya yenye inatuma baamini kama kuko kitu yenye haiko halali mu gari. Usipinge kwa kinguvu.
- Bapolisi banaweza kukuamuru weye na basafiri bako mutoke mu gari yako kwa ajili ya usalama yao. Tii maagizo kwa utulivu kama umeombwa kufanya vile.



### KAMA AFISA WA UHAMIAJI ANAKUSIMAMISHA:

- Afisa wa uhamiaji akikusimamisha, hauna haja ya kutambulisha batu bengine benye bako mu gari isipokuwa weye dereva tu. Kama maafisa banakuuliza uko na nani mu gari, unaweza jibiya: "Aba ni basafiri bangu."
- Afisa wa uhamiaji anaweza kukuamuru weye na basafiri bako mutoke mu gari yako kwa kwa ajili ya usalama yao. Tii maagizo kwa utulivu kama umeombwa kufanya vile.
- Afisa wa uhamiaji akipenda kukagua gari yako, anaweza kufanya vile kama iko tu na barua ya upekuzi yenye ilisainiwa na muamuzi mukubwa wa jimbo ao wa serikali (hapana muamuzi wa uhamiaji).
- Afisa wa uhamiaji anaweza kukukamata alama za bidole yako kama iko na uhakika kama umevunja sheria za uhamiaji.